# CLASS 5 HOLIDAY HOMEWORK TERM 2 2020

# KISWAHILI

## JUMA LA KWANZA - JUMATATU

**A. Kamilisha salamu hizi.**

1. U mzima ? ______________________
2. U hali gani ? ______________________
3. Habari za utokako ? ______________________
4. Habari za mchana ? ______________________
5. Je m wazima ? ______________________

**B. Tumia neno la heshima.**

1. Mwenye mimba .______________________
2. Mama amezaa .______________________
3. Mtoto anahara .______________________
4. Natalie nataka kalamu .______________________
5. Nimetoka kukojoa . ______________________

## JUMA LA KWANZA - JUMANNE

**A. Tumia kiulizi '-pi' vizuri.**

1. Ni kikombe ____________ kilichovunjika ?
2. Ni mtoto ____________ aliyepata zawadi ?
3. Kucheza ____________ kunafaa ?
4. Darasa ____________ halijafagiliwa ?
5. Mama alileta mifuko ____________ ?

**B. Tumia –enye au –enyewe.**

1. Mtoto ____________ kisu amefika.
2. Kiranja ____________ amejileta.

3. Mwalimu ______________ daftari hili ni yule.

4. Shimo ____________ limejaa.

5. Uteo ____________ maji umeanguka.

## JUMA LA KWANZA - JUMATANO

**A. Toa jibu mwafaka.**

1. Sakafu ya juu ya nyumba huitwa ________________.
2. Halo halo mpaka pwani ________________________.
3. Shimo lililo ukutani la kuwekea vitu huitwa ______________.
4. ______________ hutandazwa sakafuni kama mkeka.
5. Kiti kikubwa sebuleni huitwa sofa au ________________.

**B. Tumia kiulizi 'ngapi'.**

1. Watoto ______________ wamefukuzwa ?
2. Uliniletea mikate ______________ ?
3. Kalamu ________________ zimeisha wino ?
4. Madarasa ______________ yameoshwa ?
5. Babu alileta meza ________________ ?

## JUMA LA KWANZA - ALHAMISI.

**A.**

1. Vazi la kike ambalo huvaliwa kuanzia kiunoni huitwa ____________.
2. Vazi la kike linalovaliwa kifuani kusetiri maziwa huitwa ____________.
3. Kofia nyekundu huitwa ______________.
4. Vazi linalovaliwa ili kuzuia mavazi yasichafuke huitwa bwelasuti au __________ au ____________.
5. Taja vazi moja linalovaliwa na wasichana na wavulana ______________.

**B. Tumia kirejeshi 'amba' ifaavyo.**

1. Kiatu ____________ kililetwa ni kipya.
2. Miwani ____________ alivaa ni mieusi.
3. Maji ____________ ameyanywa ni machafu.
4. Watoto ____________ walifaulu mtihani wamepata zawadi.
5. Barabara ____________ hazina lami hutatiza msimu wa mvua.

## JUMA LA PILI - JUMATATU

**A. Tumia –ote au –o-ote.**

1. Kinyozi alinyoa nywele ________________________.
2. Niitie mtoto ______________________ nimtume.
3. Mama ameyanywa maziwa ____________________.
4. Kusoma _____________ hakusaidii.
5. Paka ameyanywa maziwa _______________.

**B. Tumia – enyewe.**

1. Chati ____________ ni mpya.
2. Kipepeo ___________ amepaa.
3. Manukato ___________ ni mengi.
4. Kope ____________ hunifaa.
5. Magari _____________ ni ya Tumbokarai.

---

## JUMA LA PILI - JUMANNE

**A. Toa jibu sahihi.**

1. Mmea unaotupa dawa ya wadudu huitwa ______________.
2. Mmea unaotupa sukari huitwa _______________.
3. Mmea unaotupa kahawa huitwa _____________. Pia ni aina ya ndege.
4. Mmea unaotupa ndizi huitwa ______________________
5. Mmea unaotupa mchele huitwa ______________.

**B. Tegua vitendawili hivi.**

1. Mlima sipendi. ____________________________
2. Mgeni asiyependwa . ______________________
3. Ala lakini hanenepi. ________________________
4. Mwanangu katagia mibani. _________________
5. Ninacho lakini sikitumii. ____________________
6. Kutoa ni kuongeza . ________________

# JUMA LA PILI - JUMATANO

**A. Toa wingi wa sentensi hizi.**

1. Gari lake zuri limepanda mlima.

_______________________________________________

2. Kiatu chake kipya kimekatika.

_______________________________________________

3. Manukato yake yananuka fee.

_______________________________________________

4. Uwanja wake unapendeza.

_______________________________________________

5. Unywele wake ni mweusi.

_______________________________________________

**B. Kanusha sentensi.**

1. Kauleni amefika.

_______________________________________________

2. Shule ya Johari inapendeza.

_______________________________________________

3. Mwalimu Eric yu mzima.

_______________________________________________

4. Mimi nimekula wali.

_______________________________________________

5. Gari lao lilipata ajali juzi.

_______________________________________________

E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

## JUMA LA PILI - ALHAMISI

**A. Andika maneno haya katika udogo.**

1. Mtu – ____________________
2. Kisu – ____________________
3. Meza – ____________________
4. Kiti – ____________________
5. Mti – ____________________

**B. Andika vitenzi hivi katika hali ya kutendea au kufanyia.**

1. Soma – ____________________
2. Andika – ____________________
3. Tembea- ____________________
4. Pika – ____________________
5. Kata – ____________________

## JUMA LA PILI - IJUMAA

**A. Kamilisha methali hizi.**

1. Ngoja ngoja ____________.
2. Kikulacho ____________.
3. Mgaagaa wa upwa ____________.
4. Ahadi ____________.
5. Hasira za mkizi ____________.

**B. Kamilisha tashbihi hizi.**

1. Mwaminifu kama ____________.
2. Mpole kama ____________.
3. Mrefu kama ____________.
4. Iga kama ____________.
5. Kigeugeu kama ____________.

## JUMA LA TATU - JUMATATU

**A. Andika tarakimu hizi kwa maneno.**

1. 10001 – ______________________________
2. 11000 – ______________________________
3. 100000 – ______________________________
4. Kondoo 3303 – ______________________________
5. Vitabu 2208 – ______________________________

**B. Tambua akisami hizi .**

1. $^{1}/_{8}$ – ______________________________
2. $^{2}/_{3}$ – ______________________________
3. $^{1}/_{7}$ – ______________________________
4. $^{1}/_{9}$ – ______________________________
5. ¼ - ______________________________

## JUMA LA TATU - JUMANNE

**A.**

1. Msimu wa mvua ya rasharasha huitwa vuli au ________________.
2. Wakati wa joto jingi huitwa ______________ .
3. Msimu wa mvua nyingi huitwa ______________ .
4. Kipindi cha baridi kali huitwa ______________ .
5. Wakati wa jua kali mimea ________________ .

**B. Tumia mfano huu.**

**Tunda la pili.**

1. Uteo ______________________.
2. Mlima ______________________ .
3. Kipepeo _________________ .
4. Pua _________________ .
5. Kalamu _______________ .

E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

## JUMA LA TATU - JUMATANO

**A. Toa wingi wa maneno haya.**

1. Mtume ____________________.
2. Bata ____________________.
3. Mkunga (samaki) ____________________.
4. Chati ____________________.
5. Chapati ____________________.

**B.**

1. Malipo ya kusomea huitwa ____________________.
2. Malipo ya kusafiria huitwa ____________________.
3. Malipo ya kuolea huitwa ____________________.
4. Malipo ya mwezi huitwa ____________________.
5. Malipo ya kuingia eneo Fulani kama mbuga ya wanyama huitwa ____________________.

## JUMA LA TATU - ALHAMISI

**A. Tambua nomino kundi.**

1. Tita la ______________.
2. Bunda la ______________.
3. ______________ ya miaka.
4. ______________ wa wafu.
5. ______________ ya nyota.

**B. Andika vitenzi hivi katika hali ya kutendewa.**

1. Panga ______________.
2. Kataa ______________.
3. Kimbia ______________.
4. Soma ______________.
5. Nena ______________.

E-mail: infosnkenya@g

## JUMA LA TATU - IJUMAA

**A. Unda nomino kutokana na vitenzi.**

**Mfano**

**Lima – mkulima.**

1. Pika – ______________________
2. Kimbia – ______________________
3. Cheza – ______________________
4. Chora – ______________________
5. Iba – ______________________

**B. Msamiati wa ufundi.**

1. Fundi wa mbao anaitwa ______________________.
2. Yeye hufanyia kazi katika ______________________.
3. ______________ ni kifaa cha kupimia uefu wa kitu.
4. ______________ kukerezea mbao.
5. Msumari wenye nesi huitwa skrubu au ______________________.

# Jaribio la Kwanza

***Chagua jibu sahihi kujaza mianya 1-15 katika kifungu kifuatacho.***

Msimu ___1___ kiangazi ulikuwa ___2___ . Majani ya miti yalikauka kwa kukosa maji. Wanyama ___3___ hawakuachwa nyuma. Wengi ___4___ walikufa kwa sababu ya kukosa maji na lishe. Wanadamu nao walikonda kama ___5___ . Hakuna kitu chochote ___6___ kilisazwa na ukame ___7___ . Msimu wa masika nao ___8___ sana. Kwa ___9___ mrefu, mvua haikuwa ___10___ . Kila mmoja ___11___ alitamani sana msimu wa mvua kuu uanze ___12___ watu pamoja na wanyama ___13___ lishe. Sura ya ___14___ ilibadilika na kuwa ya kutamausha. Hapo ___15___ nilipotambua kuwa maji ni uhai maishani.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. ya | B. la | C. mwa | D. wa |
| 2. | A. umeanza | B. limeanza | C. imeanza | D. utaanza |
| 3. | A. nayo | B. nao | C. naye | D. nalo |
| 4. | A. wao | B. wenu | C. yao | D. zao |
| 5. | A. mshipi | B. mti | C. ng'onda | D. sindano |
| 6. | A. ambalo | B. ambacho | C. ambayo | D. ambao |
| 7. | A. huyo | B. hao | C. hio | D. huo |
| 8. | A. ilikawia | B. ilichelewa | C. ulichelewa | D. zilichelewa |
| 9. | A. mda | B. muda | C. siku | D. wiki |
| 10. | A. imenyesha | B. umenyesha | C. limenyesha | D. mmenyesha |
| 11. | A. wenu | B. wao | C. yetu | D. wetu |
| 12. | A. ili | B. iwapo | C. kwani | D. lakini |
| 13. | A. wapate | B. mpate | C. zipate | D. kipate |
| 14. | A. nji | B. nchi | C. inchi | D. inji |
| 15. | A. ndipo | B. ndio | C. ndilo | D. ndiko |

***Kutoka swali* la 16 *mpaka* 30, *jibu kulingana na maagizo.***

16. Maana ya msemo '*kula mwata*' ni
    A. kujawa na mori
    B. kushushwa cheo
    C. kupata ufanisi
    D. pata tabu.

17. Chagua sentensi iliyoakifishwa vizuri.
    A. Sholei, Lari na Marimba ni marafiki wa dhati.
    B. Sholei, Lari, na Marimba ni marafiki wa dhati.
    C. Sholei, Lari na Marimba ni marafiki wa dhati.
    D. Sholei, Lari, na Marimba, ni marafiki wa dhati.

18. Ni neno gani lisilofaa katika orodha hii?
    A. Jezi
    B. Zulia
    C. Shubaka
    D. Dari

19. Elfu tisini na tisa mia sita na tisa kwa tarakimu ni
    A. 99 906 B. 99609
    C. 96606 D. 90699

...mosikenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

20. Chagua sentensi iliyo na kiambishi '*ki*' cha udogo;
   A. Kisu chenye makali ni hiki
   B Kila nimtembeleapo simpati
   C. Kijibwa chenyewe kilifia majini
   D. Kiatu hicho ni kizuri sana.

21. Tumia kivumishi cha kipekee '**ote**' kujaza nafasi.
   Maji _______yametumiwa kupikia.
   A. yoyote B. lote
   C. zote D. yote


22. Andika wingi wa: ***Jembe lenye makali ni hili***
   A. Majembe yenye makali ni haya
   B. Jembe zenye makali ni hizi
   C. Majembe zenye makali ni hizi
   D. Jembe yenye makali ni hizi.

23. Ni kitenzi gani kilicho katika kauli ya kutendewa?
   A. Chochea B. Tilia
   C. Pigia D. Fuliwa

24. Kamilisha sentensi kwa jibu sahihi
   Mimi _______niliyetumwa sokoni.
   A. ndiye B. ndimi
   C. ndio D. ndinyi

25. Ni kifaa kipi kati ya hivi hakipatikani katika karakana?
   A. Utepe B. Parafujo
   C. Upote D. Nyundo

26. Umbo hili huitwaje?



   A. Mistari sambamba
   B. Mistari shazari
   C. Mistari zigizagi
   D. Mistari sulubu

27. Kanusha sentensi: ***Tutaimba wakati wa sherehe.***
   A. Hatuimbi wakati wa sherehe
   B. Hatutaimba wakati wa sherehe
   C. Hatukuimba wakati wa sherehe
   D. Hatujaimba wakati wa sherehe

**28.** Chagua kivumishi cha idadi katika sentensi hii:
***Miti michache ilipandwa siku hiyo.***

A. hiyo B. ilipandwa
C. michache D. miti

**29.** Jaza pengo kwa kutumia kirejeshi '-amba'
Mfuko ______ulipotea ni wako.

A. ambao
B. ambayo
C. ambawo
D. ambazo

**30.** Ni sentensi gani iliyo sahihi kisarufi?

A. Wewe ndiyo utakaotuzwa.
B. Nyinyi ndiwe mtakaoimba.
C. Sisi ndiyo tutakaofagia
D. Yeye ndiye aliyefika.

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali*** **31 – 40**

Jumba la kongamano shuleni mwetu lilijaa watu mithili ya siafu. Ilikuwa ni siku ya wazazi shuleni mwetu. Mwendo wa saa mbili za asubuhi, wazazi wote, wake kwa waume, walianza kufululiza shuleni. Nasi wanafunzi tulikuwa tumemaliza matayarisho yote na kila kitu kilionekana nadhifu. Tuling'ara kwa sare zetu ambazo zilikuwa safi bila doa lolote. Kila aliyetuona alijua kuwa tulikuwa tayari kwa shughuli zote za siku hiyo.

Mwendo wa saa tano za asubuhi , mgeni wa heshima, ambaye alikuwa ni mkuu wa elimu jimboni mwetu, aliwasili shuleni. Sote tulimlaki kwa shangwe vifijo na nderemo. Tulipiga makofi na kuimba nyimbo za kutumbuiza. Waliandamana na mwalimu mkuu hadi ofisini mwake, kisha wakaungana na wazazi walimu na wanafunzi baadaye ili kutekeleza shughuli ya siku hiyo. Tulituzwa tuzo mbalimbali katika nyanja za elimu, michezo na usafi wa mazingira. Ilikuwa ni siku ambayo sitaisahau aushini mwangu.

**31.** Shughuli iliyotajwa katika taarifa ilitokea wapi?

A. Kanisani
B. Sokoni
C. Shuleni
D. Ofisini

**32.** '......lilijaa watu mithili ya siafu'. Huu ni mfano wa

A. nahau
B. tashbihi
C. fumbo
D. methali

**33.** Wazazi walianza kuingia shuleni saa ngapi?

A. Saa mbili
B. Saa tatu
C. Saa moja
D. Saa nne

34. Neno 'sare' katika taarifa linamaanisha
A. nguo za kuchezea
B. nguo ambazo ni mpya
C. mavazi rasmi ya shule
D. mavazi meupe

35. Mgeni wa heshima alikuwa ni
A. gavana wa jimbo
B. mwalimu mkuu
C. mmojawapo wa wazazi
D. mkuu wa elimu jimboni

36. Mgeni wa heshima alilakiwa kwa njia zifuatazo ila
A. kuimba nyimbo
B. kukunja sura
C. kupiga makofi
D. vifijo na nderemo

37. Wafuatao walihudhuria hafla iliyotajwa ila
A. walimu
B. wazazi
C. wanafunzi
D. madaktari

38. Ni nani aliyeandamana na mgeni wa heshima?
A. Mwalimu wa zamu
B. Naibu wa mwalimu mkuu
C. Mwalimu mkuu
D. Mwakilishi wa wazazi

39. Neno '**tulimlaki**' katika taarifa lina maana ipi?
A. Tulimkaribisha
B. Tulimliza
C. Tulimsuta
D. Tulimtukuza

40. Kichwa kifaacho taarifa hii ni:
A. Umuhimu wa elimu
B. Siku ya wazazi shuleni mwetu.
C. Sherehe nyumbani mwetu
D. Sherehe za sikukuu

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali* 41 – 50**

Tunapofanya jambo lolote maishani, ni sharti tuwe na **lengo**. Mtu ambaye hana lengo maishani hawezi kupata ufanisi. Kwa mfano, pale mkulima anapopanda mbegu ardhini, lengo lake huwa ni kupata mavuno ya kuridhisha hatimaye. Lengo la dereva nalo huwa ni kumfikisha **abiria** mahali anapokwenda. Naye daktari hua na lengo la kuhakikisha kuwa amempa mgonjwa tiba anayostahili kumpa ili apone au apate nafuu.

Vivyo hivyo, lengo kuu la mwanafunzi anapoenda shuleni huwa ni kupata ufanisi katika masomo. Elimu nayo humfaidi mwanafunzi aliye tayari kuipokea. Aghalabu elimu humwezesha mwanafunzi kujieleza kwa ufasaha mbele ya watu, kujikimu maishani na pia kuwa mtu mwenye maadili. Mtu akiwa na maadili, yeye huepa vitendo viovu kama vile wizi, uasherati, utumiaji wa mihadarati na kadhalika. Hivyo basi, ni muhimu sana tuwe na lengo wakati tunapotekeleza jambo fulani.

**41.** Neno jingine lenye maana sawa na **lengo** ni
- A. nia
- B. wito
- C. upendo
- D. shughuli

**42.** Mtu asipokuwa na lengo maishani hatapata
- A. aibu
- B. pongezi
- C. ufanisi
- D. shukrani

**43.** Mkulima huwa na lengo la
- A. kutopata mavuno
- B. kupata maradhi
- C. kupata mvua
- D. kupata mavuno

**44.** Neno 'abiria' katika taarifa linamaanisha
- A. watu wanaosafiri kwa gari
- B. dereva wa matwana
- C. watu wanaotembea
- D. watu wanaoendesha magari

**45.** Lengo la daktari huwa ni kumfanya mgonjwa
- A. afe
- B. apone
- C. atamaukwe
- D. akonde

**46.** Elimu humfaidi mwanafunzi
- A. aliye wa utovu wa nidhamu
- B. mwenye kiburi
- C. aliye tayari kuifaidi
- D. asiyejua maana yake

47. Elimu humwezesha msomi kufanya haya yote ila
   A. kujieleza kwa ufasaha
   B. kuwa na maadili
   C. kujikimu maishani
   D. kuwa na kiburi
48. Ni kitendo kipi kiovu hakijatajwa katika taarifa?
   A. Kutumia mihadarati
   B. Ubakaji
   C. Kuiba
   D. Uasherati
49. Lengo la mwanafunzi kuenda shuleni ni
   A. kupata ufanisi
   B. kuzua kero
   C. kujua wizi
   D. kucheza sana
50. Kichwa kifaacho taarifa hii ni
   A. Manufaa ya elimu
   B. Njia za usafiri
   C. Umuhimu wa kuwa na lengo
   D. Maadili katika jamii

---

## Jaribio la Pili

***Chagua jibu sahihi kujaza mianya 1-15 katika kifungu kifuatacho.***

Rehema ni mwanafunzi wa darasa ___1___ tano . Ana bidii kama ya mchwa ajengaye ___2___ . Husoma kwa bidii ___3___ hapendi kushika ___4___ pale anapofanya mtihani ___5___. Isitoshe, yeye ni kielelezo ___6___ kwa wenzake kitabia. ___7___ na kuwa mwenye bidii, Rehema ni mwanafunzi mwadilifu, ___8___ mwenye nidhamu. Daima, hapendi kujihusisha na wanafunzi ___9___ na tabia mbovu kwani anafahamu fika kuwa nazi mbovu ___10___.

Anapotoka shuleni kila ___11___, Rehema huwasaidia wazazi ___12___ kufanya kazi za pale nyumbani kama vile kuosha nguo, vyombo na kupiga nyumba ___13___ . Nao wazazi humpa ushauri ___14___ manufaa sana kwake. Daima, wao humkumbusha kuwa asiyesikia la mkuu ___15___.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. za | B. ya | C. cha | D. la |
| 2. | A. kichuguu | B. kombe | C. mzinga | D. zeriba |
| 3. | A. ili | B. kwa sababu | C. mpaka | D. kama |
| 4. | A. mguu | B. kichwa | C. mkia | D. tumbo |
| 5. | A. wowote | B. lolote | C. yoyote | D. chochote |
| 6. | A. njema | B. kibora | C. vyema | D. bora |
| 7. | A. Isitoshe | B. Mradi | C. Bali | D. Mbali |
| 8. | A. ila | B. tena | C. licha | D. kwani |
| 9. | A. walio | B. waliye | C. waliyo | D. walie |
| 10. | A. huuzwa ghali | B. haina faida | C. kamwuzie mjinga | D. harabu ya nzima |
| 11. | A. alfajiri | B. macheo | C. jioni | D. usiku |
| 12. | A. yake | B. wake | C. zake | D. lake |
| 13. | A. deki | B. pasi | C. rangi | D. sakafu |
| 14. | A. mwenye | B. yenye | C. wenyewe | D. wenye |
| 15. | A. hujuta majuto | B. hupata mjukuu | C. huvunjika guu | D. hupata taabu |


***Kuteka swali la 16 mpaka 30, jibu kulingana na maagizo.***

16. Ni ipi si zana ya vita?
    A. Upote    B. Uta
    C. Manati    D. Patasi

17. Mavazi rasmi yanayovaliwa na wanafunzi shuleni huitwa
    A. jezi    B. sare
    C. joho    D. bulibuli

18. Andika umoja wa: Wazee wenye hekima watatuzwa
    A. Wazee wenye hekima mtatuzwa.
    B. Mzee wenye hekima atatuzwa.
    C. Mzee mwenye hekima watatuzwa.
    D. Mzee mwenye hekima atatuzwa.

19. Alama hii ya barabarani inamaanisha



    A. mzunguko
    B. njia panda
    C. kuna mteremko
    D. hakuna kuegesha gari

20. Kanusha sentensi : Tukila wali huo tutashiba sana.
    A. Tusipokula wali huo hatutashiba sana.
    B. Tusipoula wali huo hatutashiba sana
    C. Tukila wali huo hatutashiba sana.
    D. Tusipokula wali huo tutashiba sana.

21. Jaza pengo kwa maneno yafaayo.
    Mtu _____mzigo _____ni huyu.
    A. mwenye, yenyewe
    B. enye, wenyewe
    C. mwenye, mwenyewe
    D. yenye, yenyewe

22. Kamilisha methali : Usiwatukane wakunga
    A. kabla ya kuvuka mto
    B. mambo kangaja huenda yakaja
    C. usije kujuta baadaye
    D. na kizazi kingalipo

23. Ni nomino ipi haijalinganishwa kikamilifu na ngeli yake?
    A. Kifuu - Ki-Vi    B. Kibogoyo - Ki-Vi
    C. Mtoto - A - Wa    D. Barabara - I - Zi

24. Chagua kivumishi cha sifa katika sentensi hii;
Mtoto mlafi alikila chakula chote.
A. chakula
B. chote
C. mlafi
D. mtoto

25. Ni upi si uundaji sahihi wa nomino kutokana na kitenzi?
A. Upishi - mapishi
B.Panda - upanzi
C.Lima - kilimo
D.Andika - mwandishi

26. Ni sentensi ipi iliyoakifishwa vizuri?
A. Rehema rafiki yangu ni mkristo.
B. Mbona unamliza mtoto hivyo.
C. Machungwa, maembe, na ndimu ni matunda.
D. Jina lako ni nani?

27. Chagua tashbihi isiyo sahihi
A. Takatifu kama malaika.
B. Aminika kama mchana.
C. Safi kama nyota
D. Mpole kama njiwa

28. Jibu la salamu 'makiwa' ni
A. tunayo
B. asante
C. binuru
D. alamsiki

29. Tumia 'ote' kujaza pengo.
Vitanda _______ ni vipya
A. zote
B. yote
C. nyote
D. vyote

30. Chagua sentensi iliyo sahihi kisarufi.
A. Mimi ndiwe niliyetumwa.
B. Mtu huyu ndiye mgeni wa heshima.
C. Sisi ndiye tuliyeimba vizuri.
D. Wewe ndiyo utakayetuzwa.

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali* 31 – 40**

Fuso na Bobi walikuwa marafiki wa kufa kuzikana. Walifaana kwa jambo lolote, wakati wa mvua na ule wa jua. Waama wanakijiji wote **waliwavulia kofia** kwa sababu ya kuudumisha urafiki wao. Hata hivyo, wanaume hao wawili, ambao pia walikuwa majirani, walikuwa na **hila** moja tu. Nalo ni kuwa walikuwa hawajaoa. Waliishi maisha ya upweke ijapokuwa walishirikiana vizuri. Walikuwa wenye bidii na walivuna vinono kutokana na kazi ya ukulima walioifanya. Wakati mmoja wao alipotaka kuenda safari, alimkabidhi mwenzake mali yake ili amlindie. Tabia hii iliendelea kwa **miaka ayami** bila bugudha yoyote. Hata hivyo, Fuso alianza kupatwa na tamaa.

Siku moja, Bobi alikuwa na safari ya mbali. Kama kawaida alimwendea mwenzake kumkabidhi mali yake. Alimwachia sanduku la chuma ambalo alilitumia kuwekea pesa zake. Kisha akaenda safari yake. Baada ya juma moja, Bobi alirudi kutoka safarini na akamwendea rafiki yake ili ampe sanduku lake. Hata hivyo, mwenzake alimfahamisha kwa huzuni, " panya walilivamia sanduku lako, wakalia pamoja na pesa zilizokuwa ndani"? Bobi alipandwa na mori kwani alijua kuwa mwenzake alikuwa akimchezea akili. Hata hivyo, hakuzungumza chochote, ila alinyamaza na akarudi kwake.

Baada ya siku chache, Fuso alikuwa na safari ya kuenda mjini. Aliwachukua ng'ombe wake wawili akawakabidhi rafikiye Bobi, ambaye aliahidi kuwachunga. Aliporudi kutoka safarini, Fuso alienda kuwachukua ng'ombe wake. Rafikiye alimjibu " nasikitika kukujulisha kuwa ng'ombe wako wote wawili waliliwa na mwewe" Fuso alishangaa kuwa mwewe angeweza kumla ng'ombe ilhali yu hai. Hata hivyo, hakuuliza swali kwani alijua kuwa mwenzake alikuwa akilipiza kisasi.

**31.** Sentensi ya kwanza inaashiria kuwa Fuso na Bobi walikuwa
A. marafiki walaghai
B. marafiki wasioaminiana
C. marafiki wa dhati
D. adui wa kufa kuzikana

**32.** Maneno 'waliwavulia kofia' katika taarifa yanamaanisha
A. waliwaogopa B. waliwaheshimu
C. waliwachukia D. waliwapongeza

**33.** Ni kasoro gani ambayo Fuso na Bobi walikuwa nayo?
A. Hawakuwa wameoa
B. Walikuwa wavivu
C. Walienda safari za mbali
D. Walipenda anasa

**34.** Bobi na Fuso walifanya kazi ya
A. udereva B. uvuvi
C. utabibu D. kilimo

**35.** Ni jambo lipi marafiki hawa walifanya wakati mmoja wao alikuwa na safari?
A. Kila mmoja alifungia mali yake kwake.
B. Kila mmoja alimkabidhi mwenzake mali yake amlindie
C. Kila mmoja alienda bila kumjulisha mwenzake.
D. Kila mmoja alifanya shughuli yenyewe kuwa ya siri

**36.** Maneno '**miaka ayami**' katika taarifa yamaanisha
A. miaka michache B. miaka kumi
C. miaka mingi D. miaka mitano

37. Bobi alitumia sanduku kwa kazi gani?
A. Kuwekea nafaka
B. Kuwekea chakula
C. Kuhifadhi nguo
D. Kuwekea pesa

38. Fuso alikosa kumpa mwenzake sanduku lake kwa madai kuwa
A. lilikuwa limeliwa na panya
B. lilikuwa limeliwa na mwewe
C. lilikuwa limeibwa na wezi
D. lilikuwa limepotea kimiujiza

39. Bobi alikasirika kwa sababu
A. mwenzake hakuwa ametunza sanduku lake vyema
B. alijua kuwa mwenzake alikuwa akimdanganya
C. mwenzake pia alipanga safari
D. Fuso aliiba mavuno yake

40. Kutokana na taarifa hii, tunajifunza kuwa
A. kilimo ni kazi yenye faida
B. hatufai kuwaacha watu kulinda mali yetu
C. safari za mbali hazifai kamwe
D. tunapaswa kuwa marafiki waaminifu

***<u>Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali</u>* 41 – 50**

Wahenga walisema kuwa heshima si utumwa. Hivyo basi, hatupaswi kulichukulia jambo hili kama jukumu kubwa kwetu. Kujiheshimu na pia kuwaheshimu wengine ni jambo muhimu maishani. Jamii ambayo watu wake huheshimiana huwa na maendeleo yasiyo na kifani. Hebu tujiulize. Je, ingekuwaje iwapo hakungekuwa na heshima katika jamii? Mambo yangekuwa ya kustaajabisha. Watu wangewaua wengine, waibe mali ya wenzao na wakoseane mazungumzo halisi.

Kwa mfano, watoto wana <u>wajibu</u> wa kuwaheshimu wazazi wao nyumbani. Hili huweza kutekelezwa kwa kutii maagizo. Pia, watoto hawapaswi kuwazungumzia wazazi kama watu wa **<u>hirimu</u>** yao. Wanapaswa kufanya hivyo kwa kutumia maneno ya heshima. Nao wazazi wakiheshimiwa wasijigambe ila pia wao warudishe mkono kwa kuwaheshimu wanao pia. Wasiwatese wala kuwadhulumu kwa kuwanyima chakula, matibabu,elimu, mazingira bora na kadhalika. Heshima ya watoto isiishie pale nyumbani bali iendelezwe mahali popote watoto waendapo. Kwa mfano, wakiwa shuleni wazazi wao huwa ni walimu. Hivyo basi, wawape na heshima na taadhima kuu. Wafanye lile waambiwalo kikamilifu. Njiani, watoto wawaamkue wakuu wao kwa heshima wala wasipishane njia nao kama bubu bila kunena lolote, hata salamu. Wazazi nao sharti watekeleze jukumu lao la kuwafundisha wanao heshima tangu utotoni.

41. Jamii hufaidika vipi watu wanapoheshimiana?
A. Huwa na wizi mwingi
B. Huwa na mauaji ya halaiki
C. Huwa na maendeleo mengi
D. Watu huwadharau wengine

42. Neno '**wajibu**' katika taarifa linamaanisha
A. jukumu B. tatizo
C. hamu D. sheria

43. Vitendo vifuatavyo husababishwa na ukosefu wa heshima katika jamii ila
A. mauaji ya watu
B. kusalimiana kwa taadhima
C. wizi wa vitu vya wengine
D. ukosefu wa mazungumzo mema

44. Neno '**hirimu**' limepigiwa mstari katika taarifa. Linamaanisha
A. miaka B. watoto
C. rika D. wavyele

45. Watoto huonyesha heshima kwa wazazi wao kwa
A. kutenda kinyume na maagizo
B. kuzungumza kwa utukutu
C. kukataa masomo
D. kutii maagizo yao

46. Mwandishi anawashauri wazazi warudishe shukrani kwa
A. kuwaheshimu wanao pia
B. Kujigamba mbele ya watu
C. kuwadhulumu watoto
D. kujipiga kifua

47. Watoto huweza kudhulumiwa kwa njia hizi ila
A. kunyimwa matibabu
B. kunyimwa elimu
C. kunyimwa mihadarati
D. kunyimwa chakula

48. Kulingana na taarifa, watoto wanapaswa kudhihirisha heshima
A. nyumbani pekee
B. mahali popote waendapo
C. shuleni tu pekee
D. wanapopishana njia tu

49. Mwandishi anasema kuwa watoto wanapaswa kufunzwa kuwa na heshima
A. kuanzia utotoni mwao
B. wanapoenda shuleni
C. wanapofikia utu uzima
D. wanapojua kuongea

50. Kichwa kifaacho taarifa hii zaidi ni
A. Jukumu la wazazi
B. Haki za watoto
C. Umuhimu wa salamu
D. Heshima katika jamii

E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com